WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 72 | Novemba 1 - 31 2025



# TULINDE MIUNDOMBINU YA UMEME - MHE NDEJEMBI

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**
Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**
Dkt. James Mataragio

**MHARIRI MKUU**
Neema Chalila Mbuja

**MHARIRI MSAIDIZI**
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Felista Charles
Petro Mwanda
Judith Hasani

**WAPIGA PICHA**
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo

**MSANIFU KURASA**
Brian Mbaga


© NISHATI 2025



# NISHATI SAFI YA KUPIKIA
# OKOA MAISHA
# NA MAZINGIRA

# WAZIRI NDEJEMBI AHIMIZA WANANCHI KULINDA MIUNDOMBINU YA UMEME

- Asisitiza utunzaji wa mazingira pamoja na vyanzo vya maji
- Asisitiza pia ulinzi na usalama wa miundombinu ya umeme.



Mhe. Waziri Ndejembi pamoja na viongozi wengine mbalimbali wakati wa ziara yake ya kwanza ya kutembelea mradi wa bwawa la kufua umeme wa Julius Nyerere-JNHPP

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi amewahimiza wananchi kuhakikisha ni jukumu la kila mwananchi kushiriki katika kuitunza na kuilinda miundombinu ya umeme, ili kuepusha hasara kwa serikali na usumbufu wa huduma muhimu zinazotumia nishati ya umeme.

Waziri Ndejembi amebainisha hayo wakati wa ziara yake ya kwanza ya kutembelea mradi wa bwawa la kufua umeme wa Julius Nyerere-JNHPP wa megawati 2115 Mkoani Pwani, kwa lengo la kuona maendeleo ya mradi huo.

Akiwa katika ziara hiyo Mhe. Ndejembi amesisitiza pia utunzaji wa mazingira na kuhifadhi vyanzo vya maji, ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa muda mrefu.

" Serikali imewekeza fedha nyingi takribani Shilingi trilioni 6.558 ili kuhakikisha watanzania wanapata umeme wa kutosha na wa uhakika wakati wote, hivyo tuone namna gani bora ya kulinda vyanzo vyetu tukishirikiana na TFS pamoja na TAWA, sambamba na kushirikiana na wizara nyingine kama Kilimo, maji pamoja na mifugo " Alisema Mhe. Ndejembi.



Mradi wa bwawa la kufua umeme wa Julius Nyerere-JNHPP wa megawati 2115 Mkoani Pwani.

Aliongeza kuwa kwa kufaya hivyo tutaweza kuboresha na kutunza miundombinu hiyo bila kuathiriwa na shughuli za kibinadamu kwenye mradi huu, na kutunza vyanzo vya maji ili mradi uweze kudumu na kuendelea kupata umeme wa uhakika.

Aidha Mhe. Ndejembi amesisitiza suala zima la ulinzi na usalama kwa kuongeze nguvu katika ulinzi wa miundombinu ya mradi wa JNHPP, huku akitoa wito kwa wakandarasi pamoja na viongozi kujenga utaratibu imara wa ufuatiliaji kwa kuwa mradi huo unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa umeme wa uhakika kwa kiwango kikubwa, hivyo kuimarisha uchumi wa nchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO) Bw. Lazaro Twange ameeleza kuwa mitambo ya uzalishaji umeme JHNPP imekamilika na imeanza kuzalisha megawati 950 ambazo zinatosheleza mahitaji yaliyopo na hivyo kupunguza Mgao wa umeme huku akieleza kuwa shirika linaendelea kujenga njia za kusambaza umeme ili kupeleka umeme wa uhakika kwa wananchi.

"Baada ya kukamilika kwa asilimia 100 ya ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP), Serikali imehamishia nguvu kubwa katika ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ili kuunganisha mikoa mbalimbali nchini". Amehimiza Bw. Twange

Katika ziara hiyo Mhe. Ndejembi ameambatana na Naibu Katibu Mkuu Dkt. James Mataragio, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero Mhe. Dustun Kyobya, wataalamu kutoka Shirika la umeme Tanzania(TANESCO), pamoja na Wataalamu wengine wa wizara ya Nishati.

# WAZIRI NDEJEMBI AKABIDHIWA OFISI NA ALIYEKUWA NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI DKT. BITEKO



Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi na aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko wakikabidhiana Ofisi.

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi, amekabidhiwa rasmi ofisi na aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwenye ofisi za Wizara zilizoko mtumba mkoani Dodoma, na kumshukuru Mhe. Biteko kwa utendaji wake wa kazi katika kipindi chote cha uongozi wake.

Waziri Ndejembi amesema katika kipindi cha uongozi wake, utendaji kwenye sekta ya nishati umekuwa kwa kiasi kikubwa na huduma za utendaji zimeboreshwa na tija kuonekana katika harakati za kukuza sekta ya nishati.

Waziri Ndejembi ameahidi atayaendeleza yote pale alipoishia Mhe.Biteko, ili kuhakikisha azma ya serikali na maono iliyonayo kufanikisha miradi ifikapo 2030 yanafikiwa.

Kwa upande wake, Mhe. Dkt. Biteko amempongeza Mhe. Deogratius Ndejembi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nishati na kumhakikishia kumpa ushirikiano wakati wowote katika kufanikisha maono makubwa ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Sekta ya Nishati.

“ Mengi niliyojifunza kipindi nikiwa Wizara ya Nishati lakini jambo kubwa zaidi ni sala zangu kwenu katika utekelezaji wa kazi zenu za kila siku “ amesema Biteko.

Halfla ya Makabidhiano hayo imehudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba, pamoja na viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati.



Picha ya Pamoja ya Viongozi Mara baada ya makabidhiano ya Ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.



# MHA. LUOGA AZINDUA UTAFITI WA MATUMIZI YA NISHATI KATIKA KAYA, WA MWAKA 2023.

- Asema tukio hili ni hatua muhimu katika juhudi za Serikali
- Atoa pongezi kwa timu zote zilizoshirikiana na NBS kuandaa ripoti hii.



Picha ya Pamoja katika Hafla ya Uzinduzi wa ripoti ya utafiti wa matumizi ya Nishati katika kaya wa Mwaka 2023, uliofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Takwimu Jijini Dodoma.

Kamishina wa Umeme na Nishati Jadidifu Mha. Innocent Luoga kutoka Wizara ya Nishati , amezindua Takwimu za Matumizi ya Nishati katika Kaya kwa mwaka 2023.

Hafla hiyo imefanyika katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu Jijini Dodoma.

Kamishina Luoga amefanya uzinduzi huo leo wakati akimwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba ambapo amesema kuwa tukio hilo ni hatua muhimu katika juhudi za Serikali kuhakikisha tunapata takwimu sahihi na za kuaminika kuhusu namna Watanzania wanavyotumia aina mbalimbali za Nishati majumbani mwao ikiwa ni pamoja na umeme, gesi, kuni, mkaa na Nishati jadidifu kama vile nishati ya umeme wa jua na Upepo

Vilevile, Kamishina ameeleza ripoti hiyo ni matokeo ya ushirikiano wa karibu kati ya ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Wizara ya Nishati pamoja na taasisi zake, kwa ufadhili na usaidizi wa kiufundi na utaalam kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) kupitia Expertise France. Ameeleza“ Napenda kutoa pongezi kwa timu zote zilizoshiriki katika utafiti huu zilizoshirikisha wataalam wa takwimu na watafiti wa Nishati kwa kazi nzuri na ya kitaalam inayofanikisha kupatikana kwa ripoti hii muhimu”.

Aidha, Mha. Luoga amesema asilimia 52.7 ya kaya nchini zinatumia umeme kama chanzo cha Nishati. Hata hivyo, matokeo yanaonesha tofauti kubwa kati ya maeneo ya mjini na vijijini ambapo matumizi ya umeme mijini ni



asilimia 72.7 wakati vijijini ni asilimia 30.7 pekee.

Sambamba na hilo Kamishina amesisitiza kuwa ripoti hii imebainisha kuwa asilimia 66 ya kaya hutumia kuni, asilimia 44 hutumia mkaa, wakati asilimia 25 inatumia gesi ya LPG, na asilimia 2 zinatumia umeme kwaajili ya kupikia. Hii inaonesha bado kuna nafasi kubwa ya kuelimisha na kuhamasisha Wananchi kuhusu matumizi ya Nishati safi na salama ya kupikia, ili kulinda afya, mazingira na rasilimali zetu za misitu.

Kwa upande wa Nishati kwa Maendeleo ya Viwanda Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa Umeme wa uhakika na wa gharama nafuu kupitia Miradi mikubwa ya kimakakati kama Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) ambalo limekamilika kwa asilimia 100 na kuwezesha upatikanaji wa umeme wa jua na upepo hivyo kusaidia kupanua mtandao wa gridi ya taifa ili kufikia viwanda vyote vidogo na vikubwa katika mikoa yote.

Kwa muktadha huo Mha. Luoga ameongeza kuwa Serikali itaendelea kutumia matokeo ya Utafiti huu kama nyenzo muhimu katika kupanga na kutekeleza sera bora za Nishati, zinazolenga kuhakikisha kila Mtanzania anapata Nishati ya uhakika, nafuu na endelevu.

Naye, Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dkt. Amina Msengwa ameishukuru Wizara ya Nishati na taasisi zake zote kwa ushirikiano wao kwa kipindi chote cha kuandaa takwimu hizi lakini pia amemwomba Kamishna wa umeme na Nishati Jadidifu Mha. Innocent Luoga kuwa miradi hii ya kuandaa ripoti za utafiti wa matumizi ya Nishati katika kaya iwe endelevu, kwani itatusaidia katika utekelezaji wa Sera na mikakati madhubuti.

Pia, Mhe. Anna Makinda, Spika Mstaafu na Kamisa wa Sensa 2022, ametoa shukrani za dhati kwa wageni wote walioshiriki katika uzinduzi wa Utafiti wa Matumizi ya Nishati katika Kaya amesema kupitia ripoti hii tunatakiwa kuchukua hatua kama tutafanikiwa kutumia nishati safi itatusaidia kutunza muda na mazingira yetu kwa ujumla.

"Naipongeza Wizara ya Nishati na Tasisi zake pamoja na wadau mbalimbali lakini pia Wananchi waliotoa taarifa hizi kwani itatusaidia kuongeza matumizi ya nishati safi na kuachana na Nishati zisizo salama", Ameongeza Mhe. Makinda.



# WIZARA YA NISHATI YAKUTANA NA WADAU WA TEKNOLOJIA YA NISHATI SAFI.

- Lengo ni kufahamu changamoto za uzalishaji, usambazaji na upatikanaji wa Teknolojia ya Nishati safi.
- Wadau ni chombo muhimu ili kufika 80% ifikapo 2034.



Picha ya pamoja Katika Ufunguzi wa kikao na wadau mbalimbali wa Nishati safi ya Kupikia Jijini Dar es salaam.

Wizara ya Nishati kupitia kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia, Imekutana na wadau mbalimbali wa uzalishaji usambazaji wa Teknolojia za nishati safi ya kupikia Jijini Dar es Salaam ili kufahamu changamoto za uzalishaji upatikanaji na usambazaji wa teknolojia ya nishati safi ya kupikia.

Lengo la mkutano huo ni kupata mapendekezo kutoka kwa wadau hao ya namna bora Serikali chini ya Wizara ya Nishati itaweza kuwasaidia wadau hao ili kufikia lengo la matumizi ya Nishati safi ya kupikia la asilimia 80 ifikapo 2034 kwa watanzania.

Katika Ufunguzi wa kikao kazi hicho na wadau hao MkurUgenzi Kitengo cha Nishati safi ya Kupikia Bw. Nolasco Mlay amesema lengo mojawapo katika malengo mahsusi ya Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ni Kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia. "tunafahamu kuwa lengo hili haliwezi kufanikishwa na Serikali pekee bila kuhusisha Sekta binafsi ambayo ndio mdau muhimu katika kuhakikisha kuwa uwekezaji kupitia uzalishaji na usambazaji wa nishati safi ya kupikia unaakisi mahitaji ya wananchi."Alisema Mlay

Kulingana na takwimu zilizozinduliwa na Tume ya Taifa ya Takwimu (NBS) Novemba 2025 zinaonesha ongezeko la matumizi ya nishati safi nchini limefikia asilimia 23.2%, hivyo kutokana na ongezeko hilo Wizara chini ya kitengo cha Nishati safi imeona ipo haja ya kukutana na wadau ili kuona namna serikali itashirikiana na wadau kukidhi ongezeko hilo.

Ni dhahiri kuwa ongezeko hili la mahitaji linapaswa kwenda sambamba na upatikanaji,uzalishaji na usambazaji wa nishati hizi ili kuwa na usawa katika mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia. "Suala la Nishati safi ya kupikia ni suala mtambuka na kila mmoja anapaswa kushiriki na kushirikishwa ili kufikia lengo ambapo amewapongeza wadau mbalimbali kwa michango yao katika jitihada za kuhakikisha nishati safi ya kupikia inamfikia kila mtanzania na michango yao katika kujenga Taifa lenye tija, afya bora mazingira salama na uchumi jumuishi.

Naye mmoja wa wadau na msambazaji wa Teknolojia ya Nishati safi (Kuni Smart) kutoka Jijini Mwanza Bw. Bernard Makachia amesema kwamba kikao kazi hiki kilichoandaliwa na Wizara ya nishati kimekuja kwa wakati muafaka na kitasaidia wadau mbalimbali wanaojihusisha na Teknolojia Nishati safi mchini kuweza kuwasilisha changamoto zao ili kufikia lengo la kitaifa kukiwa na matumaini makubwa kwamba zitafanyiwa kazi kwa wakati na kuongeza kuwa Sekta binafsi ni mdau mkubwa wa Nishati Safi hivyo akishiriikiana na serikali lengo la asilimia 80 litatimia ifikapo 2034.

Kikao kazi hicho na wadau mbalimbali wa nishati safi kimefanyika kwa siku mbili kikiwakutanisha wadau kutoka Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, Taasisi na Wizara za Kiserikali, Mashirika na Taasisi binafsi, Asasi za kiraia, Taasisi za Kifedha na wadau binafsi.

# HAKIKISHENI MRADI WA NJIA ZA KUSAFIRISHA UMEME ZINAKAMILIKA KWA WAKATI MHE. NDEJEMBI

- Ni baada ya kukamilika kwa kituo chakupokea na kupoza umeme cha Chalinze.
- Lengo ni Kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa kutosha Nchini.



Waziri wa Nishati Mhe. Deogratius Ndejembi pamoja na viongozi wengine katika Ziara yake ya kukagua njia za kusafirisha umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma ikiwa ni baada ya kukamilika kwa mradi wa Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Julius Nyerere(JNHPP).

Waziri wa Nishati Mhe. Deogratius Ndejembi amemtaka Mkandarasi anayetekeleza mradi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma kuhakikisha kuwa kazi za njia za kusafirisha umeme zinakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Ndejembi ameyasema hayo Mkoani Pwani wakati akiendelea na ziara yake ya kukagua njia za kusafirisha umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma ikiwa ni baada ya kukamilika kwa mradi wa Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Julius Nyerere(JNHPP).

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi katika kutekeleza mradi huu na imedhamiria kuboresha miundombinu ya umeme nchini ili kuongeza upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa wananchi na sekta za uzalishaji, hivyo tuhakikishe hadi Juni 2026 mradi huu uwe umekamilika". Amesisitiza Mhe. Ndejembi.

Aidha Mhe. Ndejembi amesisitiza kuwa ubora wa kazi lazima uzingatiwe ili miundombinu iweze kudumu kwa muda mrefu na kufanya kazi kwa ufanisi ili wananchi wapate umeme wa kutosha huku akiwataka TANESCO kuweka maridhiano na wakandasi hao pamoja na kuhakikisha rasilimali zote muhimu zinapatikana kwa wakati ili utekelezaji wa mradi huo uendelee kwa uharaka zaidi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO) Bw. Lazaro Twange ameeleza kuwa Serikali ya Jamuhuri ya muungano wa Tanzania imewekeza fedha zaidi ya Trilioni 13.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo 5 vya kupokea na kupooza umeme pamoja na vituo 35 vya njia za kusafirisha umeme.

"Baada ya kukamilika kwa Bwawa la kufua umeme la JNHPP tunaendelea na ujenzi wa vituo na njia za kusafirishia umeme kutoka JNHPP Mpaka Chalinze ambapo kuna kituo cha kupokea na kupoza umeme na badae kuusafirisha mpaka kituo cha Zuzu Dodoma ambacho kitaharakisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Dodoma ,Singida, Tabora na Mikoa mingine ya jirani."Ameeleza Bw. Twange

Katika Ziara hiyo Mhe. Waziri Ndejembi aliambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Dkt. James Mataragio, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero Mhe. Dunstan Kyobya, Mkuu wa Wilaya ya Chalinze, Wataalamu kutoka TANESCO pamoja na Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati.



# NAIBU WAZIRI MAKAMBA ASISITIZA UWEPO WA MAGHALA YA KUHIFADHIA MAFUTA NCHINI.

- Ataka kuwepo njia ya haraka ya usafirishaji wa Mafuta
- Asisitiza uwezekano wa kupunguza gharama za ununuzi wa vifaa vya mifumo ya umeme majumbani (wiring)
- Asisitiza uwepo wa Fursa kwa makundi ya Vijana ili kuwajengea uwezo.

Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati Mhe. Salome Makamba ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuimarisha njia bora na ya haraka ya usafirishaji wa Mafuta nchini ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa mafuta.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Makamba alipofanya kikao kazi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Jijini Dodoma.

Mhe. Makamba amesisitiza uwepo wa maghala ya kutosha ya kuhifadhia mafuta Nchini ili Wananchi waepukane na changamoto ya ukosefu wa Mafuta na kupongeza jitihada za kukabiliana na changamoto hii ambayo wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuidhibiti.

Sambamba na hilo Mhe. Makamba ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuangalia namna bora ya upunguzaji gharama za Vifaa vya uwekaji wa mifumo ya umeme majumbani ili kuongeza Idadi ya watumiaji wa Nishati hiyo hasa maeneo ya vijijini.



Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati Mhe. Salome Makamba alipotembelea na kufanya kikao kazi na (EWURA)

Vilevile Mhe. Makamba amesisitiza Mamlaka hiyo kuangalia namna bora ya kutoa fursa mbalimbali hasa kwa kundi la Vijana ili kupunguza wimbi kubwa la Vijana wasiokuwa na ajira nchini Tanzania na kuwashirikisha fursa mbalimbali zilizoko kwenye sekta ya nishati nakuwajengea uwezo kwenye miradi.

Nae Dkt. James Andilile Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ameeleza kazi mbalimbali zinazofanywa na mamlaka hiyo ikiwa ni pamoja na Kudhibiti Ubora, Usalama na tija ya watoa huduma vilevile kutathimini na kurekebisha bei za huduma. Sambamba na vipaumbelee watavyoyovisimamia ndani ya siku ya miamoja ikiwa ni kutekeleza agizo la Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Sisi kama Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji tutaendelea kuweka mizania ya maslahi sawa kati ya Wadau husika na hivyo kuchochea ongezeko la tija, ushindani, na upatikanaji wa huduma bora kwa wote lakini pia tutaendelea kuzingatia misingi mikuu ya Utawala bora katika maamuzi ya Udhibiti ambayo ni weledi, uwajibikaji, Utabirikaji, Ushirikishwaji wa wazi na kufuata Sheria." Amesema Dkt. Andilile.



Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali waliohudhuria katika kikao kazi kilichoongozwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba na menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Jijini Dodoma.

# WAZIRI NDEJEMBI AWATAKA PBPA KUHAKIKISHA KUNAKUWEPO NA AKIBA YA KUTOSHA YA MAFUTA NCHINI

- Ahimiza uboreshaji wa Miundombinu ya kupokelea mafuta
- Ahimiza kutokuwepo na ucheleweshaji kwenye uingiaji wa mafuta nchini.
- Alekeza ushirikishwaji wa Wadau katika kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia mafuta




Mhe. Waziri Ndejembi alipotembelea ofisi za PBPA Jijini Dar es Salaam ikiwa nimuendelezo wa ziara yake ya kuzungumza na viongozi wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Nishati.

Waziri wa Nishati Mhe. Deogratius Ndejembi amewataka Wakala wa Kuagiza Mafuta kwa Pamoja( PBPA) kuhakikisha kunakuwepo na akiba ya kutosha ya mafuta nchini lengo likiwa ni kuhakikisha uendelevu wa shughuli za uzalishaji, usafirishaji na huduma nyingine muhimu ambazo zinategemea kwa kiasi kikubwa nishati hiyo

Mhe. Ndejembi ameyasema hayo Jijini Dar es salaam katika ofisi za PBPA ikiwa nimuendelezo wa ziara yake ya kuzungumza na viongozi wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Nishati

Ametoa maelekezo kwa PBPA kuhakikisha akiba ya mafuta hapa nchini inakuwa ya kutosha kwani itasaidia kuepuka uhaba wa ghafla unaoweza kusababisha ongezeko la gharama kwa wananchi na sekta binafsi na kukosekana kwa huduma hiyo.

"Akiba ya mafuta ya kutosha kupitia uwekezaji katika vituo vya kuhifadhi kunaleta utulivu wa kiuchumi kwa Taifa kwani kunapokuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta, shughuli za uzalishaji, usafirishaji na biashara zinaendelea bila vizuizi na hii huongeza imani ya wawekezaji, hupunguza gharama za dharura,



Picha ya pamoja ya Viongozi mbalimbali katika ofisi za PBPA Jijini Dar es salaam.

na hatimaye kukuza ukuaji endelevu wa uchumi".Amesisitiza Mhe. Ndejembi

Aidha Mhe. Ndejembi amewataka viongozi wa PBPA kuhakikisha wanawekeza zaidi katika kuimarisha miundombinu ya kupokelea mafuta na kuhifadhia mafuta ili kuboresha usalama na ubora wa bidhaa kwa maslahi mapana ya Taifa

Sambamba na hilo Mhe. Ndejembi amesisitiza wakala hao kushirikiana na wadau wa sekta binafsi kwenye mnyororo wa usambazaji mafuta lengo likiwa ni kuhakikisha upatikanaji wa maghala ya kuhifadhia mafuta ili kuondoa ucheleweshaji wa mafuta au upungufu usiotarajiwa.

Awali akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa kuagiza mafuta kwa pamoja Bw. Erasto Simon ameeleza kuwa Katika kuhakikisha ufanisi katika utendaji kazi PBPA imejiandaa kuunganisha mifumo itakayosaidia kutoa bei linganifu kwenye bandari zote ili kuleta ufanisi katika usambazaji wa mafuta.

Katika ziara hiyo, Mhe. Ndejembi ameambatana na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba pamoja na watalaamu wengine wa wizara.

# WANANCHI MIKOA YA IRINGA NA DODOMA KUWA NA UMEME WA UHAKIKA - MHE. MAKAMBA.

- Atembelea mradi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Mtera
- Awaasa wananchi kutunza mazingira ili kulinda vyanzo vya maji.
- Zaidi ya Bilioni Kumi zimetumika kutekeleza miradi hii.




Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba alipotembelea na kukagua mradi wa kuzalisha umeme kwa njia ya maji la Bwala la Mtera liliopo mpakani kati ya Iringa na Dodoma, ambapo amesema kuwa wananchi wa mikoa ya Dodoma na Iringa sasa kuwa na umeme wa uhakika.

Mhe. Makamba amesema Mitambo ya kufua umeme imeboreshwa kwa kiasi kikubwa sana na mitambo hii inauwezo wa kuzalisha umeme mpaka ifikapo msimu ujao wa mvua na hii ni habari njema kwa wananchi wa wilaya ya Mpwapwa,Chamwino na Isimani .

“ Kimsingi mitambo hii mara baada ya kuboreshwa inatuhakikishia kuwa umeme unapatikana wa kutosha hivyo kwa ujumla mikoa ya Dodoma na Iringa itakuwa na umeme wa uhakika”.Alisema Mhe. Makamba

Aidha Mhe Makamba aliongeza kuwa juhudi hizi za Serikali lazima tumshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amehakikisha anasikiliza changamoto za wananchi na kuzitatua.

Amesema hadi kukamilika kwa mashine hizi mbili jumla ya zaidi ya shilingi Bilioni Kumi zimetumika katika kurekebisha na kutengeneza mitambo hii ya kuzalisha umeme.

Sambamba na hilo Mhe. Makamba ametoa rai kwa wananchi wanaozunguka vyanzo vya maji ambavyo ni chanzo cha Bwawa la Mto Mtera ikiwemo wananchi waishio pembeni mwa bonde la Ihefu kulinda vyanzo hivyo kwa sababu nishati ni uti wa ngongo wa uchumi wa Tanzania.

Kwa Upande wa Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazaji wa umeme TANESCO Mha. Athanasius Nangali ameeleza kuwa kituo kinafanya kazi vizuri na kituo hiki kinaendelea kuzalisha Megawati 80 kama ilivyokuwa awali.

Amewataka Wananchi waendelee kuwekeza katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kutokana na umeme unapatikana kwa uhakika na hii inatokana na kukamilika kwa kituo cha kupokea na kupoza umeme kipya kilichojengwa kutokana na usimamizi wa wakala wa nishati vijijini (REA).



# MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA SIO ANASA-MHE. MAKAMBA.

- Asema Nishati safi ya kupikia ni kipaumbele cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Taasisi zaidi ya Hamsini zenye idadi ya watu 100 na zaidi kupelekewa nishati safi ya kupikia.
- Vitongoji 9000 kufikiwa ndani ya muda mfupi Tanzania.




Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali wakati wa ziara Mhe. Salome Makamba alipokutana na Bodi ya Wakala wa Nishati Vijini (REA),katika Ofisi za REA zilizopo jijini Dodoma, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake kwenye taasisi zilizoko chini ya Nishati.

Imeelezwa kuwa matumizi ya Nishati safi ya kupikia sio anasa bali ni muhimu kwa kutunza mazingira na afya za wananchi,na pia inasaidia kupunguza muda wa uzalishaji ambapo kwa sasa wananchi wanatakiwa kuhama katika tamaduni za kubaki kutumia nishati isiyo safi na kutumia nishati safi ya kupikia.

hayo yameelezwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba alipokutana na Bodi ya Wakala wa Nishati Vijini (REA),katika Ofisi za REA zilizopo jijini Dodoma, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake kwenye taasisi zilizoko chini ya Nishati.

“Natoa rai kwa watanzania kuwa matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia sio anasa bali kwanza yanasaidia kutunza mazingira , pili yanasaidia kupunguza muda wa uzalishaji ambao mwanamke anakaa jikoni muda mrefu kupika wakati ukitumia nishati safi na inaokoa zaidi ya asilimia 70% ya muda ambao unatumia kupika”.

Aidha, amesisitiza kwa wananchi wote kubadilika na kwenda na wakati sambamba na kwenda na kasi ya Dunia inavyoenda,ambapo kwa sasa matumizi ya kuni na matumizi ya Mkaa kwa sehemu kubwa ya dunia hawatumii kabisa, hivyo tunatakiwa kwenda kwa kasi hiyo ili watu wote watumie nishati safi ya kupikia.

Nishati safi ya kupikia ni kapaumbele cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivyo kama serikali inaendelea kutoa ruzuku ili kuhakikisha wananchi wanapoenda kujaza au kunua mitungi gesi bei inakua punguful, pia Serikali inaweka juhudi kubwa kuhakikisha vituo vya ujazaji wa gesi katika mitungi inakua karibu na wananchi walipo.

Aidha, Mhe. Makamba ameongeza kuwa mipango mingi ambayo Serikali imejiwekea ipo ile mingi ambayo ni ya muda mfupi na michache ya muda mrefu, lengo likiwa ni kuendelea

kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais ya kuwafikishia wananchi umeme kwenye vitongoji.

Ameongeza kuwa Wizara ya Nishati kupitia REA inaendelea kutekeleza mpango wa kuvifikia vitongoji 9000 kwa kipindi hiki kifupi na kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika.

Sambamba na hilo Mh. Rais amekua kinara wa Nishati safi ya kupikia na amezungumzia sana juu ya suala hili katika majukwaa mbalimbali , hivyo basi kwa upande wa nishati safi ya kupikia Wizara kupitia REA ndani ya muda huu mfupi imeandaa mradi wa muhsusi kuhakikisha taasisi zaidi ya hamsini (50) zinapata nishati safi ya kupikia na hizi ni taasisi ambazo zina idadi ya watu kuanzia 100 na zadi, ili kuweza kupunguza uharibifu wa mazingira pamoja na kuokoa muda ambao taasisi zinatumia kwa ajili ya kutengeneza chakula.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya wakala wa nishati vijijini- REA Mha.Hassan Said amesema kuwa mpango wa serikali ni kuhakikisha kasi ya kuwaunganishia umeme wananchi katika vitongoji unakua endelevu na kuongeza kuwa hali ya upatikanaji wa umeme inaongezeka.

Amesema jumla ya vitongoji vilivyopo nchini ni 64,359 kati ya hivyo vitongoji 39,000 tayari vimepatiwa umeme ikiwa ni sawa na asilimia 60% vilivobakia ni vitongoji 25,400 kati ya hivyo vitongoji 2,500 miradi inaendelea wakati vitongoji 9,000 Wakala upo katika hatua ya mwisho ya utiaji saini ili vifikishiwe umeme.

Aidha Mhe. Naibu waziri alifanya ziara ya kufanya ziara kutembelea Kituo cha kupoza na kusafirisha umeme cha Zuzu kwenda kujionea hali ya kituo,kazi inayofanyika sambamba na hatua za ujenzi iliyofikiwa kwa baadhi ya maeneo ya kituo hicho zinavyoendelea.

# MHE.NDEJEMBI ASISITIZA USHIRIKIANO KWA VIONGOZI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YENYE KIPAUMBELE KWA WANANCHI.

- Ahimiza kufanya kazi kwa kushirikiana na Wadau
- Ahimiza kufanyika kwa tafiti mbalimbali hasa katika gesi na mafuta
- Akutana na Taasisi za PURA na TPDC

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb), ametoa wito kwa viongozi na watendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kuhakikisha wanaimarisha ushirikiano katika kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati inayogusa moja kwa moja ustawi wa wananchi.


Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi pamoja na viongozi wengine walipotembelea na kufanya kikao na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Akizungumza Jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kikazi ya mazungumzo na viongozi wa bodi na menejimenti za taasisi hizo, Mhe. Ndejembi alisisitiza ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya kupaumbele kwa Taifa kwani Serikali inategemea utendaji wa weledi, uwajibikaji na uwazi kutoka kwa taasisi hizo ili kuhakikisha miradi ya kimkakati inatekelezwa kwa wakati na kwa viwango vya kimataifa.

"Napenda kumshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa nafasi hii, nimeona ni vyema kukutana nanyi kwa






Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi pamoja na viongozi wengine walipotembelea na kufanya kikao na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

lengo la kufahamiana, kujifunza lakini pia kuhakikisha tunaweka sawa mikakati mathubuti katika utekelezaji wa majukumu yetu lakini pia kuhakikisha tunaongeza kasi na bidii katika kutekeleza majukumu yetu ili kuongeza upatikanaji wa nishati ya uhakika nchini". Amesisitiza Mhe. Ndejembi.

Waziri Ndejembi pia amewataka viongozi wa TPDC na PURA kuhakikisha wanazipitia changamoto zinazoathiri kasi ya utekelezaji wa miradi na kuwasilisha mapendekezo ya maboresho yatakayowezesha kuongeza tija huku akisisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa ufanisi hasa katika kipindi hiki ambapo Serikali imewekeza nguvu kubwa katika kukuza miundombinu ya nishati na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Aidha, aliwahimiza viongozi kuendelea kujenga utamaduni wa kushirikiana na wadau mbalimbali kufanya tafiti mbalimbali hasa katika mafuta na gesi kwani sekta ya mafuta na gesi ina ushindani mkubwa duniani na hivyo inahitaji uongozi thabiti, mipango madhubuti na matumizi bora ya rasilimali ili kuhakikisha Tanzania inanufaika ipasavyo na rasilimali zake.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Petroli Tanzania Mussa Makame amemshukuru Waziri kwa ziara hiyo na kuahidi kuendelea kuboresha mifumo ya utendaji pamoja na kuimarisha ushirikiano wa taasisi kwa maslahi mapana ya Taifa huku akiahidi kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha malengo ya taifa yanafikiwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mhandisi Charles Sangweni ameeleza namna taasisi hiyo ilivyojikita Katika kuanzisha vyanzo vya mapato huku akiahidi kutekeleza yote yaliyoagizwa pamoja na kuongeza uwazi katika usimamizi wa miradi kwa kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi za maendeleo ya miradi ya nishati inayotekelezwa nchini.

**PICHA MBALIMBALI ZIKIONYESHA WATUMISHI WA WIZARA YA NISHATI WAKIFANYA MAZOEZI YA KUIMARISHA AFYA KATIKA VIWANJA VYA OFISI ZA WIZARA HIYO ILIYOKO MJI WA SERIKALI MTUMBA, JIJINI DODOMA.**











**PICHA MBALIMBALI WAKATI MKURUGENZI MSAIDIZI SEHEMU YA RASILIMALI WATU, BI. BAHATI MTONO, AKIFUNGUA MAFUNZO YA E-UTENDAJI, E-OFFICE NA ULINZI WA MTANDAO (ICT SECURITY) KWA WATUMISHI WA KITENGO CHA HUDUMA ZA SHERIA, KITENGO CHA TEHAMA, PAMOJA NA IDARA YA UTAWALA NA RASILIMALI WATU, YALIYOFANYIKA KATIKA OFISI YA WIZARA YA NISHATI, ILIYOPO MJI WA SERIKALI MTUMBA JIJINI DODOMA.**









# ELIMU YA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YATOLEWA KWA MAAFISA DAWATI NA WARATIBU WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KATIKA HALMASHAURI NA MIKOA YOTE NCHINI.



Elimu ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia inayotolewa na Wizara ya Nishati kwa maafisa dawati na waratibu wa nishati safi ya kupikia katika halmashauri na mikoa yote nchini, inatarajiwa kuokoa vifo vya watu zaidi ya 33,000 kila mwaka vinavyotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

Hayo yameelezwa na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia Wizara ya Nishati, Mhandisi Banezeth Kabunduguru wakati akiwasilisha mada katika mafunzo ya maafisa hao yaliyofanyika mkoani Singida.

Mha. Kabunduguru amefafanua kuwa, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 takribani watu 33,024 hufariki kila mwaka nchini Tanzania kutokana na athari za matumizi ya nishati isiyosafi ya kupikia.

“Zaidi ya watu milioni 3 duniani hufariki kutokana na athari za matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia ambapo asilimia 60 ya vifo hivi ni wanawake na watoto”. Amesema Mha. Kabunduguru.

Amesisitiza kuwa kati ya vifo 500,000 hadi 700,000 hutokea Afrika na kwa Tanzania watu 33,024 hufariki kila mwaka hivyo elimu inayotolewa inalenga kuongeza kasi ya uelewa kwa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya Nishati Safi ya kupikia na hivyo kupunguza vifo hivyo.

Akizungumza kwa niaba ya maafisa dawati, kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Iramba Mkoani Singida, Yohana Dondi na Getrude Lamshai kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Meru mkoani Arusha wamesema kuwa elimu waliyoipata itawawezesha kuratibu kwa ufanisi utekelezaji wa ajenda ya nishati safi katika maeneo yao.

Wamesema kuwa, elimu hiyo itasaidia kuongeza taasisi na kaya zinazotumia nishati safi, kubadilisha mitazamo ya jamii, na kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

“Kwa kuwa ajenda ya nishati safi ni mtambuka, tutaishirikisha jamii, taasisi, na wadau wote ili kuhakikisha tunapata matokeo chanya na kupunguza utegemezi wa nishati zisizo salama kama kuni na mkaa,” alisema Dondi.

Kupitia elimu hii, jamii inatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa athari za kiafya, kimazingira, kijamii na kiuchumi zinazosababishwa na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Pia, elimu hii itachochea maendeleo ya sekta ya nishati safi nchini na kusaidia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya

Nishati Safi ya Kupikia 2024–2034.

Maafisa dawati na Waratibu kutoka halmashauri na mikoa ya Dodoma, Singida, Arusha, Kilimanjaro na Manyara wameshiriki katika mafunzo ya siku moja ya Matumizi ya nishati safi ya kupikia mkoani Singida.














For more info
www.nishati.go.tz